



## JUMUIYA YA KIMATAIFA LA KIHUDUMA WA KANISA LA MUNGU (LINALOTUNZA SIKU YA SABA)

Ramon Ruiz	Rais	<a href="mailto:imc-president@cog7.org">imc-president@cog7.org</a>
Bryan Cleeton	Mkurugenzi Mkuu	<a href="mailto:imc-director@cog7.org">imc-director@cog7.org</a>
Whaid Rose	Naibu wa Kwanza wa Rais	<a href="mailto:imc-vicepresident1@cog7.org">imc-vicepresident1@cog7.org</a>
Jorge Gillig	Naibu wa Pili wa Rais	<a href="mailto:imc-vicepresident2@cog7.org">imc-vicepresident2@cog7.org</a>
Lawyer Obara	Mweka Hazina	<a href="mailto:imc-treasurer@cog7.org">imc-treasurer@cog7.org</a>
John Klassek	Katibu	<a href="mailto:imc-secretary@cog7.org">imc-secretary@cog7.org</a>

<https://imc.cog7.org>

Tarehe: Januari 11, 2020

Wapendwa Wandugu na Wadada Katika Kristo kote kote kwa Kanisa La Mungu (Linalotunza Siku ya Saba),

"Nilikuwa nimekufa na sasa niko hai", Haya matamshi maarufu wa Yesu, yanayonukuliwa kwenye maandiko, kwa uhakika, ndio ushuhuda wetu pia. Sisi tuliokuwa wafu kwa dhambi, sasa tuko hai ndani ya Kristo. Sisi tuliopokea Kristo na kuliadini Jina Lake, sasa tumekombolewa na kupatanishwa. Hili ni jambo linalotupasa kusifu na kufurahi! Na ndio maana kila mwaka kwa pamoja kote ulimwenguni, tunasheherekea uhalisi wa hili agano jipya linalotiwa muhuri na damu la Yesu na kuandikwa ndani ya mioyo yetu. Mwaka huu, kumbukumbu hili la Chakula Cha Jioni la Bwana litaadhimishwa mnamo tarehe 7 mwezi wa nne (Aprili), mwaka wa 2020, jioni baada ya jua kutua.

Katika Jumuiya ya Kimataifa la Kihuduma wa Kanisa La Mungu (Linalitunza Siku ya Saba) tunafanya na kusherehekea pamoja na kwa umoja, katika Jina La Bwana Yesu Kristo, kwa ajili ya utukufu wa Baba wetu wa Mbinguni. Tunatangaza maadhimisho haya ya kila mwaka kama uhuisho wa agano letu katika Kristo. Mkate unaomegwa huwakilisha mwili wa Yesu uliopondeka. Nayo kinywaji yanayotokana na matunda ya mizabibu huwakilisha damu ya Yesu iliyomwagika kwa ajili yetu. Na kwa unyenyekevu, tunatawadha miguu ya kila mmoja wetu, tukizingatia mfano ambayo Yesu mwenyewe alituwekea. Tunafanya haya kama jamii, tukijumuika kwa sababu ya hili agano jipya. Tunatangaza pia matarajio ya kurudi kwa Yesu kila mara tunapohudhuria.

Tafadhali tuma hili barua kote kote kwenye eneo/ jimbo lako. Pia agiza wachungaji wote waweze kusoma ujumbe huu muhimu kwa wakati ufaao kwa makanisa yao yote.

Katika Jina La Yesu na kwa niaba ya Jumuiya ya Kimataifa la Kihuduma,



John Klassek  
Katibu



Ramon Ruiz  
Rais



Bryan Cleeton  
Mkurugenzi Mkuu